# WAKALA WA USAJILI UFILISI NA UDHAMINI

# (RITA)

## TAARIFA KWA UMMA

## TAARIFA KUHUSU MAENDELEO YA UTEKELEZAJI WA MPANGO WA USAJILI NA KUTOA VYETI VYA KUZALIWA KWA WATOTO WA UMRI CHINI YA MIAKA MITANO KATIKA MKOA WA IRINGA NA NJOMBE ULI-OZINDULIWA TAREHE 22 SEPTEMBA 2016.

**UTANGULIZI:**

Wakala wa Usajili Ufilisi na Udhamini (RITA) umekuwa ukichukua hatua mbalimbali zenye lengo la kuhakikisha kiwango cha Usajili wa Vizazi na Vifo nchini kinaongezeka ili kuiwezesha nchi kuwa na taarifa sahihi za wananchi waliozaliwa katika ardhi ya Tanzania bara. Kwa mujibu wa Takwimu za Sensa ya mwaka 2012 ni asilimia 13 wamesajiliwa na kupata vyeti vya kuzaliwa.

RITA kwa kushirikiana na wadau mbalimbali imebuni na kuanza kutekeleza Mpango wa Usajili na Kutoa vyeti vya Kuzaliwa kwa watoto wa Umri chini ya Miaka Mitano ambao unaendelea kutekelezwa katika mikoa mitano ya Tanzania Bara ambayo ni Mwanza, Mbeya, Songwe na hivi karibuni ulizinduliwa katika Mikoa ya Iringa na Njombe. Huu ni mpango endelevu na wa kudumu katika maeneo unapotekelezwa.

Mpango huu ulibuniwa ili kuleta suluhisho la changamoto zilizokuwa zikisababisha watoto kushindwa kusajiliwa na kupata vyeti vya kuzaliwa kwa wakati ambapo msingi wake mkuu umejengwa katika Kusogeza huduma za usajili karibu na makazi ya wananchi hivyo kupatikana katika Ofisi za Watendaji Kata na Vituo vya Tiba vinavyotoa huduma ya Afya ya Mama na Mtoto. Vile vile huduma hii hutolewa Bila malipo. Taarifa za usajili huingizwa katika programu maalum iliyowekwa kwenye simu (mobile app) na kutumwa kwenye kanzidata ya wakala papo kwa papo kupitia ujumbe mfupi wa simu. Taarifa hizi huchambuliwa na mfumo wa usajili na kuonyesha idadi ya waliosajiliwa kwa jinsia, umri, kituo, kata, halmashauri na mkoa, ili kurahisisha upatikanaji wa takwimu na kufuatilia utekelezaji.

Taarifa zinazopatikana kutokana na usajili wa Vizazi ni muhimu sana kwa serikali kwani huiwezesha kupata Takwimu sahihi zinazosaidia katika kupanga mipango ya maendeleo na usambazaji wa huduma za jamii katika ngazi zote za maamuzi.

### MAFANIKIO YA UTEKELEZAJI KATIKA MIKOA WA IRINGA NA NJOMBE

Mpango wa Usajili na Kutoa Vyeti vya Kuzaliwa kwa Watoto wa Mikoa ya Iringa na Njombe ulizinduliwa Rasmi na Mhe. Harrison G.Mwakyembe -Waziri wa Mambo ya Katiba na Sheria na kuanza kutekelezwa katika halmashauri zote 11 za Mikoa hii.

Kabla ya kuanza utekelezaji Wasajili Wasaidizi ambao ni Maofisa Watendaji kata na Wahudumu wa vituo vya Tiba walipewa mafunzo ya kina ya siku tatu kuhusu Usajili wa vizazi, uhakiki wa viambatiisho, utambuzi wa walengwa, kutuma na kutunza kumbukumbu.

Kwa upande wa idadi ya Vituo, Mkoa wa Njombe una vituo vya Usajili 326 na Mkoa wa Iringa Vituo 352 ambavyo kote vitaendelea kutoa huduma hiyo kwa watoto wanaozaliwa.

Lifuatalo ni Jedwali linaloonesha Takwimu za Usajili kabla na baada ya kuanza kutekeleza Mpango huu.

| Na. | Mkoa | Idadi ya Watoto (Sensa 2012) | Asilimia watoto waliosajiliwa na kupata Vyeti Kabla ya Kuanza Mpango (Sensa | Idadi ya Watoto waliosajiliwa na Kuwa na Vyeti Baada ya kuanza Mpango (22 Septemba, 2016) | Asilimia ya Watoto waliosajiliwa na Kuwa na Vyeti Baada ya kuanza Mpango (18 Nov 2016) |
|---|---|---|---|---|---|
| 1 | Njombe | 93,248 | 8.5 | 94,270 | 98 |
| 2 | Iringa | 129,120 | 11.7 | 127,842 | 95 |

Kwa mujibu wa Takwimu hapo juu, Utekelezaji wa Mpango huu umefanikiwa sana kwani idadi ya watoto waliosajiliwa kwa mkoa wa Njombe imepanda kutoka 8.5% na kufikia 98% na Mkoa wa Iringa kutoka 11.7% na kufika 95%.

Kwa upande wa jinsia, wanawake wamesajiliwa zaidi katika mikoa yote miwili ( Njombe 50.3% na Iringa 50.4%) kuliko wanaume japokuwa tofauti kati yao ni ndogo. Vilevile Halmashauri tatu za Mji wa Mafinga, Makambako na Mji wa Njombe mpaka sasa zimeweza kuwasajili watoto wote wa umri chini ya Miaka Mitano walio katika maeneo yao kama inavyoonekana katika *kiambatisho Na 1*.

**HITIMISHO:**

Utekelezaji wa Mpango wa Usajili wa Watoto wa Umri chini ya Miaka Mitano katika Mikoa ya Iringa na Njombe umefanikiwa sana na kuweza kupita malengo ya kusajili watoto asilimia 90 kwa kipindi cha miezi sita ya Mwanzo.

Vile vile, ili kutorudia katika hali iliyokuwepo ya mlundikano wa watoto wasiosajiliwa, RITA itaendelea kufanya kazi kwa karibu na Uongozi wa Mkoa, Wilaya na wadau wengine kuhakikisha kwamba kila mtoto anasajiliwa na kupata cheti ndani ya Muda mfupi baada ya kuzaliwa.

RITA tunaamini tumeweza kufikia lengo letu kutokana na ushirikiano tulioupata kutoka kwa Waziri Mhe. Dr, Harrison Mwakyembe pamoja na uongozi wa Wizara ya Mambo ya Katiba na Sheria kwa ujumla, Wakuu wa Mikoa na Viongozi wote wa Mikoa hii Miwili ya Njombe na Iringa pamoja na wadau wa maendeleo ambao ni Shirika la Umoja wa Mataifa la KuhudumiaWatoto Duniani (UNICEF), Serikali ya Canada kupitia Shirika la Idara ya Mambo ya Nje, Biashara na Maendeleo (DFATD), Kampuni ya Simu za Mkononi ya TIGO na Shirika la Wafanyakazi wa Kujitolea (VSO). Tunawashukuru sana Tunatambua na Kuthamini mchango wao.

**Emmy Kalomba Hudson**
**Kaimu Afisa Mtendaji Mkuu - RITA**

| | ESTIMATED POPULATION (Census Data) | REGISTERED (11/17/2016) | % COVERED BY TODAY |
|---|---|---|---|
| IRINGA & NJOMBE | 231,367 | 222,112 | 96% |
| | | | |
| IRINGA REGION | 135,108 | 127,842 | 95% |
| IRINGA DC | 37,822 | 35,155 | 93% |
| IRINGA MC | 18,922 | 17,955 | 95% |
| KILOLO | 31,824 | 30,381 | 95% |
| MAFINGA TC | 9,902 | 10,516 | 106% |
| MUFINDI | 36,638 | 33,799 | 92% |
| NJOMBE REGION | 96,259 | 94,270 | 98% |
| LUDEWA | 19,147 | 18,474 | 96% |
| MAKAMBAKO | 13,479 | 16,042 | 119% |
| MAKETE | 11,938 | 9,977 | 84% |
| NJOMBE DC | 12,746 | 12,321 | 97% |
| NJOMBE TC | 16,436 | 16,406 | 100% |
| WANGING'OMBE | 22,513 | 21,041 | 93% |




